*SWAHILI FORUM 11 (2004): 171-177*

# ASILI YA MATUMIZI YA *IKO* KATIKA KISWAHILI CHA BARA[1]

URSULA DROLC

This paper speculates about the origin of the overall use of the form *iko* in Inland Swahili. Its functional scope comprises predication, identification, location, existence, and association. In Standard Swahili, the primary function of *iko* is to express the locative relation of nouns belonging to noun class 4 or 9. For the expression of identification various other means are used. As Inland Swahili is mostly acquired as a second language it will be argued here that the functional expansion of *iko* might be due to the crosslingusitic influence of the first language. However, first languages, such as Maasai, exhibit a formal distinction between location and predication. A conceptual merger of both functions in the second language is more likely to occur when the first language contains only one obligatory copula expressing both concepts. This obligatory copula can be found in many Indo-European languages, e.g. English or Hindi. Until today Indians speaking Swahili are characterised by the frequent usage of *iko*, a fact which points to the view that the overall use of *iko* could be due to substrat influence of Hindi.

Lengo la makala haya ni matumizi ya **iko** yanavyojitokeza katika Kiswahili cha bara la Afrika Mashariki. Nilikuta matumizi hayo nilipoandika tasnifu yangu ya uzamifu 'Swahili among the Maasai. On the Interlanguage Swahili by Maa Speakers'. Lengo langu lilikuwa ni utafiti wa Kiswahili kama lugha ya pili. Watu wakijifunza lugha ya pili wanapenda sana kutafsiri lugha yao ya kwanza. Ili kupata athari ya lugha ya kwanza, nilinasa mazungumzo ya watu 16. Kumi na watatu kati yao walizungumza Kimaasai kama lugha ya kwanza na waliosalia watatu wa kundi dhibitiwa (*control group*) walizungumza Kiswahili, Kichagga na Kigogo.

Kundi tafitiwa (*speaker group*) (13): L1 Maasai

Kundi dhibitiwa (*control group*) (3): L1 Swahili, Chagga, Gogo

Nilishangaa sana nilivyosikia maneno haya ya mwanamke mmoja katika kundi dhibitiwa. Alikuwa Mswahili aliyetoka Tanga, Tanzania:

(1) wa-pare iko smart

Sitaki kusema si kweli kwamba Wapare ni *smart* nadhifu lakini sarufi ya sentensi hii inashangaza sana. Kiswahili ni lugha yenye ngeli. Jina **wa-pare** linajitokeza katika ngeli ya pili inayotegemea kiambisho **-wa**. Lakini sentensi **wapare wako smart** tena si Kiswahili kizuri kabisa. Katika Kiswahili sanifu kuna njia mbalimbali za kuonyesha kiarifa (*predication*) na nomino (*noun*) au or kivumishi (*adjective*):

[1] Makala yalitolewa katika Kongamano la 17 la Kiswahili, Chuo Kikuu cha Bayreuth, tarehe 21 Mai hadi 23 Mei 2004. Tanbihi ya wahariri: Tunamshukuru sana Nathan O. Ogechi aliyejitahidi kusahihisha Kiswahili cha makala hii. Makosa yanayobaki ndiyo shauri ya mwandishi.

**Kwanza**: Kuna kopula **ni**:

(2) wapare **ni** smart /wazuri

**Pili**: Kuna vijina maalum, viwakilishi vya kiima (*subject pronouns*) ama viambishi vyenye kujenga vitenzi (*verb prefix formative*; Closs 1967, Bearth 1995). Viambishi hivi ni vizee sana na havitumiki sana.

(3) **ni** mpishi

(4) **u** nani?

(5) **tu** wapishi

**Tatu**: Kuna kopula ya sifuri (*zero copula*; Stassen 1997:62) inayofuatwa na matamshi maalum (M), yaani mnyamao kidogo baada ya jina la kwanza. Nomino na vilevile sifa, nomino huweza kuambatanishwa na vivumishi vya sifa (*adjective*) ifuatavyo:

(6) wapare (M) wakulima

(7) sahani hizi (M) safi

(8) sisi (M) tayari

**Nne**: Kitenzi **kuwa** ambacho ni lazima kiwepo ili kuunganisha nomino na viambisho vya kiwakati au kawaida:

(9) wapare **huwa** smart

**Tano**: Kionyeshi **ndiyo** kinatumika ili kusisitiza au kutofautisha.

(10) wapare **ndiyo** smart, siyo wazungu.

Swali linalobaki ni: je, kwa nini Mswahili kutoka Tanga anatumia **iko** kwa maana ya kutambulisha (*identification*) badala ya njia mojawapo hizo tano zilizoonyeshwa hapo juu? Katika Kiswahili sanifu, kionyeshi **iko** kinaunganishwa na kiambisho cha ngeli ya tisa au nne **i-** (cl. 4, 9) na kiambisho rejeshi cha ngeli ya 17 **-ko**, ndiyo ngeli ya mahali (11). Mbali na viambisho rejeshi **-po** na **-mo**, kiambisho **-ko** kinatumika kwa kurejea mahali pa kitu au mtu. Lazima kuunga na kiambisho cha ngeli (12,13) ama kiwakilishi kiima (14):

(11) sahani **i-ko** meza-ni

(12) ki-tu **ki-ko** wapi?

(13) wa-geni **wa-ko** nyumbani

(14) tu-po

Kwa sababu Kiswahili cha bara hutumiwa kama lugha ya pili, kuna lahaja mbalimbali zinazoonyesha maingiliano na lugha za kwanza. Mojawapo ni Kimaasai. Katika Kimaasai pia kuna vionyeshi tofauti vinavyorejelea kiarifu ama mahali. Tena kuna njia mbalimbali za kuonyesha kiarifu:

**Kwanza**: Kitambushi **a-rá** ‘to be sth.’ (Tucker-Mpaayei 1955:90) kinatumika na wakati wa kisasa tu. Kwa kurejea wakati wa zamani kuna kitenzi kingine :

(15) a-ra sapʊk

1Sg.-KOP kubwa

'ni mkubwa, mimi mkubwa'

(16) a-ra ɔlaɪguɛnanɪ

1Sg.-KOP kiongozi

'mimi ni kiongozi'

Pili: Kuna njia ya kopula ya sifuri (*zero copula*):

(17) nanʊ ɔlaɪguɛnanɪ

'mimi kiongozi'

(18) ɔlmalɪmuɪ nɪnyɛ

mwalimu yeye

'yeye mwalimu'

Ili kurejelea mahali, kuna kitenzi **a-tií** 'to be somewhere' (Tucker-Mpaayei 1955:90 f.). Kitenzi hicho kinatumika na vionyeshi vya wakati wo wote. Mifano (19) na (20) inaonyesha kwamba kimaasai ni lugha yenye mpangilio wa Kitenzi-Kiima-Yambwa (*VSO language*).

(19) e-tii nkishu bɔɔ

3Sg-ko ng'ombe nje.

'ng'ombe wako nje ya nyumba ndani ya manyatta'

(20) e-tii ɔpa ɔltʊŋanɪ

3Sg-ko zamani mtu

'alikuwa zamani mtu'

Pia imedhihirika kwamba Wamaasai wanatumia njia mbalimbali ili kurejea kitambulisho, kiarifu na mahali. Kwa hivyo, wajifunzapo Kiswahili huwa wameshajua tofauti zake. Wakizungumzapo Kiswahili wanatumia **iko** ili kurejea mahali:

(21) bado iko nyumbani

Sentensi hii imetamkwa na mwanamke mmoja Mmaasai asiyejua Kiswahili vizuri. Alikuwa anataka kusema kwamba mvulana wake bado anakaa nyumbani. Aliendelea na sentensi inayofuata. (Tafsiri yake kwa Kiswahili sanifu imetolewa chini yake kwa alama za kufunga na kufungua).

(22) iko shuleni darasa la saba

'anaenda shule darasa la saba'

Maana yake nyingine ni kurejelea kuweko au uhusiano:

(23) iko ndugu

'kuna ndugu au nina ndugu'

Kuna vile vile njia mbalimbali za kuonyesha kiarifu. Kwa mfano, maneno ya mama mzee mmoja. Alikuwa hakijui Kiswahili sana. Kiswahili chake kilitosha tu kwa kusalamia watu na

kuongea kidogo. Alishinda akijifahamisha maneno ya lazima lakini sarufi ya Kiswahili chake haikuwa nzuri sana. Hakuweza kutumia viambishi vya ngeli na kwa vitenzi alitumia kiambishi **na**- peke yake. Lakini yeye pia alitumia njia mbalimbali ili kutoa ujumbe wa kuarifu. Njia hizo zinafanana sana na Kiswahili sanifu:

**Kwanza**: Kuna **ni**:

(24) miti hii ni miti musuri
'mti huu ni mzuri'

**Pili**: Kuna kopula ya sifuri

(25) mimi bado siangiki (wasichana)
mimi bado msichana.

**Tatu**: Kitenzi **kuwa** pia kimetumika:

(26) mimi nakuwa koko (bibi)
mimi nimekuwa bibi.

**Nne**: Na mara moja yeye pia anatumia **iko** kwa kutambulisha:

(27) mimi iko koko yako kweli
mimi ndiyo bibi yako ya kweli

Matumizi hayo ya **iko** kwa kutambulisha hupatikana pia katika lahaja nyingine ya Kiswahili cha bara. Duran (1979:148) alifanya utafiti wa lahaja ya Kiswahili upande magharibi ya Kenya. Alisema kwamba **iko** ni kionyeshi cha Kiswahili kinachotumiwa katika Afrika Mashariki nzima kama lugha ya pili. Anaita lahaja hiyo *pidgin Swahili.* Anatoa mifano hii:

Mahali:

(28) yeye iko kwa duka

Uarifu:

(29) yeye iko tayari

Uhusishi:

(30) yeye iko na pesa

Kitabu cha kwanza kuhusu Kiswahili cha bara ni *Upcountry Swahili*. Kiliandikwa na LeBreton (1936, repr. 1968). Yeye alisema kwamba kuna aina tatu za kutafsiri *to be* kwa Kiswahili: kopula ya sifuri, alama **ni** kwa kutambulisha na kuarifu, na **iko** kwa kurejesha ujumbe wa mahali.

> "The present tense of the verb 'to be' is generally expressed either by simple omission...or by the word IKO when a stronger sense is required or position is intended. There is also a weak form NI when the verb is only a connecting link between two nouns, or between a noun and an adjective or adverb." (1936/1968:37)

Heine (1973:96) anasema kwamba kwa *Kenya Pidgin Swahili* (KPS) kuna kopula tatu: **iko**, **ni** na **ndiyo.** Matumizi yao si lazima, yaani kuna pia kopula ya sifuri. Mifano anayotoa inaonyesha matumizi ya **iko** kwa kurejea utambulishi:

> "Das KPS besitzt die drei Kopulae *iko, ni* und *ndiyo*..., die bis zu einem gewissen Grad freie Varianten bilden. Bei einigen Sprechern scheint die Tendenz zu bestehen, die drei Formen mit unterschiedlichen Graden der Emphase in Verbindung zu bringen, wobei *ndiyo* starke Emphase, *iko* weniger starke Emphase und *ni* keine Emphase ausdrückt." (1973:95)

Tunaona sasa kwamba matumizi ya **iko** kama kopula si kosa la watu ambao hawajui Kiswahili sana lakini imekuwa kionyeshi kinachopatikana sehemu mbalimbali katika bara la Afrika. Duran (1979) anakisia asili ya Kiswahili cha bara:

> "what are the origins of Kenyan pidgin Swahili? Did the English and Afrikaans-speaking Europeans who once dominated the African population of Kenya, and the Asians who operated as 'gatekeepers' to the European power-structure, have much part in the shaping of the pidgin? Or is the pidgin a survival of an earlier Swahili trade-route pidgin extending from the upper tributaries of an earlier Swahili trade-route pidgin extending from the tributaries of the Congo to the Great Lakes and the Indian Ocean? Or have the non-Bantu populations of Kenya had much part in the development for Kenyan pidgin-Swahili?" (1979:150)

Kuna maoni tofauti juu ya eneo la Kiswahili cha bara wakati wa zamani sana. Aliposafiri Afrika Mashariki Burton (1872) alisema kwamba watu walitafsiri lugha moja kwa lugha nyingine:

> "Questions and answers had to pass through three and even four media." (1872:438)

Lakini kwa wakati vilevile Thomson (1885) alisema kwamba ni muhimu sana kujifunza Kiswahili kwa sababu hutumika Afrika nzima:

> "One of the most important of these (preparations) was the study of Kiswahili, a language not only spoken by the natives at the coast, but so well-known in the interior as to enable the traveller who can speak it to pass almost from one side of Africa to the other. If by any chance he lights upon a tribe, no member of which can speak the Swahili language, he is almost certain to have among his followers one who can speak the dialect of that particular tribe." (1885:29)

Kiswahili cha bara hutumiwa kama lugha ya pili. Watu wakijifunza lugha wanafanya makosa lakini kila kosa lina habari yake. Tunaweza kutofautisha athari mbili kuu za lugha ya pili:

1. Eneo la ujumbe: Ujumlishaji na upanuzi wa matumizi.

2. Maingiliano ya lugha nyingine: Athari za mwingiliano na lugha nyingine

**1. Eneo la ujumbe.** Tuliona kwamba kwa Kiswahili sanifu, kiambishi **-ko** kinarejea mahali peke yake. Lakini Bearth (1995:228) anasema kwamba vilevile kiambishi **-ko** hutumika kwa kuarifu:

> "Einer quasi-universalen Tendenz folgend, Zustandsbeschreibungen ‚lokalistisch', d.h. nach dem Muster von Ortsprädikaten zu kodieren, verwendet das Swahili in Verbindung mit vorwiegend prädikativ gebrauchten Zustandsadjektiven gerne die Ortskopula –ko."

Anatoa mifano hii:

| | | |
|---|---|---|
| (31) yuko tayari | yu tayari | ni tayari |
| (32) (mlango) uko wazi | u wazi | ni wazi |

Namna hii inawezekana kueleza eneo la ujumbe wa **iko**. Lakini matumizi haya ya alama **-ko** kwa kuarifu yamefungwa na maneno machache ambayo yana maana ya kubadilika hali. Na vilevile bado kuna viambishi vya ngeli. Kwa hivyo, maoni hayo hayawezi kueleza matumizi ya **iko** kama kopula ya kuarifu kabisa.

**2. Athari ya lugha ya kwanza.** Watu wanapozungumza lugha ya pili, wanatafsiri maneno ya lugha yao ya kwanza. Hivyo, sarufi ya lugha ya pili inawezekana kuingiliwa na lugha ya kwanza. Kwa kueleza matumizi ya **iko** inabidi sasa kutafuta lugha ambazo zinatumia neno moja kwa ujumbe wa mahali na kuarifu.

Tulivyoona kuhusu Kiswahili sanifu na pia kuhusu Kimaasai, kuna njia mbalimbali za kurejea mahali au kuarifu. Lakini kwa lugha za Ulaya kuna alama moja tu inayorejea mahali na kuarifu. Kwa mfano kwa kiingereza *to be*:

| | |
|---|---|
| (33) S/he is here | Hairuhusiwi: she here |
| (34) S/he is smart/ a teacher | Hairuhusiwi: she smart/ she teacher |

Vile vile kwa Kihindi kuna kopula moja *hone*. Matumizi yake ni lazima kwa kurejea mahali na kuarifu. Mifano inaonyesha matumizi yake na vielezi, jina na sifa. Kopula imewekwa mwisho wa sentensi:

(34) vah yahā~ hai
3Sg hapa KOP3S
yupo hapa

(35) vah adhyāpak hai
3Sg. mwalimu KOP3S
yeye mwalimu

(36) vah sundar hai
3Sg mzuri KOP3S
yeye mzuri.

Inawezekana kwamba matumizi arifu ya **iko** yanatokea kwa watu waliozungumza lugha kama Kiingereza au Kihindi. Kuna Wahindi wachache tu waliokaa Afrika Mashariki (2% ya idadi yote ya wananchi, Nassem 1975:ii). Lakini 1890 wakati gari-la-moshi lilipojengwa kwenda Uganda, Wahindi wengi walifanya kazi huko na walianza kujenga maduka yao kila mahali

(Naseem 1975:136, 145f.). Pesa za wakati huu Maria-Theresia Dollar imebadilishwa 1898 kwa rupia[2] kwa kuraihisisha biashara ya wahindi (Naseem 1975:167).

Ili kufanya biashara ilibidi iwepo lugha ya mawasiliano. Wakachukua Kiswahili. Walipojifunza Kiswahili walitafsiri Kihindi. Walitafuta neno badala ya kopula yao *hone*. Kwa bahati nzuri, walikuta neno la **iko** na walipanua ujumbe wake. Eneo la Afrika Mashariki lina lugha nyingi tofauti na makabila mbalimbali. Watu waliokuja dukani kununua vitu kwa Mhindi walitumia Kiswahili kwa mawasiliano. Kwa sababu ya matumizi yake kama lugha ya pili Kiswahili cha bara huonyesha mwingiliano ya lugha mbalimbali. Mojawapo ni athari ya lugha Kihindi.

Mpaka sasa matumizi ya **iko** ni alama ya Kiswahili Kihindi. Kwa mfano Stanislaus Olonde huitwa Stano anatumia **iko** kwa kupambanua maneno ya Mhindi kwa vibonzo vya Gitonga. Vilevile katika kitabu cha Mohammed Said Abdulla (1977) kuna Banyiani moja anayetumia **iko** sana bila kubadilisha alama ya ngeli. Mifano yote niliyokuta inarejea mahali tu: **Nani iko? Boi iko nje** (1977:56); **ile iko biashara** (1977:58); **hii samba iko** (1977:59) **iko damu** (1977:61).

## Marejeo


Abdulla, Mohammed Said. 1977. *Mzimu wa watu wa kale*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Bearth, Thomas. 1995. Sein und Haben - kuwa na kutokuwa. *Swahili-Handbuch*, imehaririwa na Gudrun Miehe and Wilhelm Möhlig, pp. 207-239.

Burton, Richard (1872). *Zanzibar, City Island and Coast*. London:

Closs, Elisabeth. 1967. Some Copula Constructions in Swahili. *Journal of African languages* 6,2: 105-131.

Drolc, Ursula. 1999. *Swahili among the Maasai. On the Interlanguage Swahili by Maa Speakers*. München: Lincom Europa.

Duran, James. 1979. Non-standard Forms of Swahili in West-Central Kenya. (ed.) *Readings in Creole Studies*, ed. by Ian Hancock Ian. Ghent: E. Story-Scentia, pp. 129-153.

Heine, Bernd. 1973. *Pidgin-Sprachen im Bantu-Bereich*. Berlin: Dietrich Reimer Verlag.

LeBreton, F.H. 1936 (repr.1968). *Up-country Swahili. For the Farmer, Merchant, Business Man, and their Wives, and for all who deal with the Up-country African*. Richmond, Surrey: R.W. Simpson and Co.


[2] Mpaka sasa *rupia* ina maana ya ‘pesa’ kwa kimaasai.

Naseem, Abdul Waheed. 1975. *Nature and Extent of the Indian Enterprise along the East African Coast and Subsequent Role in the Development of Kenya 1840-1905*. Ann Arbor: University Microfilms International.

Olonde, Stanislaus. 1996. *Gitonga*. Nairobi: Sasa Sema Publications Limited.

Stassen, Leon.1997. *Intransitive Predication*. Oxford: Clarendon Press.

Tucker, Archibald na J. Tompo ole Mpaayei. 1955 (repr. 1986). *A Maasai Grammar with Vocabulary*. London, New York, Toronto: Longmans, Green and Co.